

TAARIFA KWA WATEJA NA WAGENI WA HUDUMA ZA WAHAMIAJI WA KITUO CHA TUUSULA KUHUSU VIRUSI VYA CORONA

Iliyoandikwa hapa ni maagizo kuu kutoka kwa Serikali kuu ya Finlande kuhusu virusi vya Corona:

Dalili za virusi vya Corona ni nini?

- homa kubwa au joto ya juu sana mwilini
- kuumwa na misuli
- kikohozi
- upungufu wa kupumua
- uchovu

Ikiwa unashuku kwamba umeambukizwa, piga simu kwenye kituo chako cha afya.

Ikiwa dalili zako zimezidi, uugua nyumbani.

- Usikutane na marafiki wala usiende kazini ikiwa una ugonjwa wa mafua au wahisi kwamba ni corona.
- Epuka au usihudhurie matukio makubwa au ya watu wengi.
- Usiwatembelee wale ambao ni wazee kwani wao ndiyo wako hatarini zaidi.

Osha mikono na ukiwa na kikohozi kohoa vizuri

Usafi mzuri ni njia bora ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa virusi vya corona na virusi vingine vyote.

- Osha mikono mara kwa mara kwa kutumia sabuni na maji.
- Ikiwa huwezi kuosha mikono yako, tumia vidonge vya mkono
- Kinga mdomo wako wakati wa kukohoa au kupiga chafya. Kwa mfano, tumia kitambaa au mkono wa nguo. Usikohoe au usipige chafya kwenye mkono wazi.

Maelezo ya jumla kuhusu virusi vya corona:

1. Virusi vya Corona haina madhara au hatari yeyote kwa watoto > jaribu kutuliza mtoto ikiwa anaogopa corona.
2. Virusi vya Corona kwa kawaida sio hatari ikiwa mtu ni wa afya mzuri kwa ujumla na hana magonjwa ya kimsingi.

3. Ikiwa mtoto wako ana dalili za mafua au homa (kamasi, kikohozi, homa) usimpeleke shuleni au kwenye huduma cha mchana cha watoto.
4. Epuka na usafiri wa umma (kama vile treni za abiria, mabasi ya msongamano, na metro) inapowezekana.
5. Chakula na mahitaji mengine ya msingi hayawezi kuisha madukani hapa Finlande. Serikali ya Finlande iko na uhfadhi yake maalum na viwanda vinaendelea kupeleka vyakula na mahitaji mengine madukani kama kawaida.
6. Kwaihvyo kila mmoja atulie, awe na amani na tusaidiane: Hivi ndivyo tutaweza kukabiliana na jambo hili.